SIKU KUMI ZA MWANZO DHUL-HIJJAH NA SIKU ZA TASHRIIQ

Fadhila na Ahkām Zake



Mwandishi
Abuu Zakariyyaa, Yahya bin Hassan Al-hanbaly

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

UTANGULIZI

Kila sifa njema ni stahiki ya Allah (Mola wa Ulimwengu wote). Sala na Salamu zimfikie Mjumbe wa Allah (Muhammad), Ahli zake, Maswahaba zake na wale wote waliowafuatia kwa wema mpaka siku ya Qiyama.

Mwezi wa Dhul-hijja ni katika miezi minne mitukufu, ambayo Allah ﷻ ameibainisha katika aya aliposema:

﴿ إِنَّ عِدَّةَ ٱلشُّهُورِ عِندَ ٱللَّهِ ٱثۡنَا عَشَرَ شَهۡرٗا فِي كِتَٰبِ ٱللَّهِ يَوۡمَ خَلَقَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضَ مِنۡهَآ أَرۡبَعَةٌ حُرُمٞۚ ذَٰلِكَ ٱلدِّينُ ٱلۡقَيِّمُۚ فَلَا تَظۡلِمُواْ فِيهِنَّ أَنفُسَكُمۡۚ ﴾ التوبة [36]

Hakika idadi ya miezi mbele ya Allah ni kumi na mbili katika Kitabu cha Allāh (Lauhul-mahfuudh) tangu siku alipoumba Mbingu na Ardhi. Ndani yake kuna miezi minne mitukufu. Hiyo ni hesabu ya sawa sawa, basi msizidhulumu nafsi zenu ndani miezi hiyo. (At-tawbah aya 36)

Miezi hii minne imatajwa kwa majina yake katika Sunna za Mtume katika Hadithi aliyosimulia Abuu Bakrah – Allāh amridhie, ya kwamba Mjumbe wa Allāh ﷺ amesema:

(إِنَّ الزَّمَانَ قَدِ اسْتَدَارَ كَهَيْئَتِهِ يَوْمَ خَلَقَ اللَّهُ السماوات وَالْأَرْضَ، السَّنَةُ اثْنَا عَشَرَ شَهْرًا، مِنْهَا أَرْبَعَةٌ حُرُمٌ، ثَلَاثٌ مُتَوَالِيَاتٌ: ذُو الْقَعْدَةِ وَذُو الْحِجَّةِ وَالْمُحَرَّمُ، وَرَجَبُ مُضَرَ الَّذِي بَيْنَ جُمَادَى وَشَعْبَانَ)

“Hakika ya zama zimeendelea kuzunguka kama kawaida yake tangu siku Allāh alipoumba Mbingu na Ardhi. Mwaka ni miezi kumi na mbili. Ndani yake kuna miezi minne mitukufu: Dhul-qa’ada, Dhul-hijja, Muharram na Rajab Mudhwara, ambao upo baina ya Jumāda na Sha’abān”[1]

Ama hekima ya Allāh ﷻ kuhusisha kutofanya dhulma ndani ya miezi hii minne, ni kama alivyobainisha Qatādah – Allāh amrehemu:

« الْعَمَلُ الصَّالِحُ أَعْظَمُ أَجْرًا فِي الْأَشْهُرِ الْحُرُمِ وَالظُّلْمُ فِيهِنَّ أَعْظَمُ مِنَ الظُّلْمِ فِيمَا سِوَاهُنَّ، وَإِنْ كَانَ الظُّلْمُ عَلَى كُلِّ حَالٍ عَظِيمًا»

“Matendo mema yana ujira mkubwa ndani ya Miezi Mitukufu, na dhulma ndani yake ni kubwa kulikoni dhulma katika miezi mingineyo, ijapokuwa dhulma katika kila hali ni jambo kubwa”[2]

Hivyo tunafaidika na Aya hii kuwa; Mwezi wa Dhul-hijja ni katika miezi minne mitukufu, na pili, kuacha kuzidhulumu nafsi zetu ndani yake kwa kufanya madhambi na kuacha twaa.

[1] Sahiihul-Bukhāry, Hadithi na. 4385
[2] Tafsiirul-baghawiy, Juzuu 2 Uk.329

Baada ya utangulizi huu, ndani ya Risala hii, nitagusia nukta zifuatazo:-

1. Fadhila za siku kumi za mwezi wa Dhul-hijjah
2. Maandalizi kabla ya kuingia Masiku Kumi ya Dhul-hijjah
3. Matendo yanayofanyika katika Siku Kumi za Dhul-Hijja
4. Siku ya Arafa
5. Siku ya ‘Eidul-adh-ha
6. Siku za Tashriiq
7. Fiqhi ya makusudio ya ibada hizi tukufu

FADHILA ZA SIKU KUMI ZA MWEZI WA DHUL-HIJJAH

1. Ni siku ambazo Allāh ﷻ ameziapia ndani kitabu chake aliposema

﴿ وَلَيَالٍ عَشْرٍ ۝٢ ﴾ الفجر [2]

“Na ninaapa kwa Masiku Kumi” (Al-fajr aya 2)

Hizi siku kumi ambazo Allāh ﷻ ameziapia ni siku kumi za mwanzo wa Mwezi wa Dhul-hijjah. Anasema Ibnu Rajab Al-hanbaly – Allah amrehemu:

فهي عشر ذي الحجة، هذا الصحيح الذي عليه جمهور المفسرين من السلف و غيرهم، وهو الصحيح عن ابن عباس (لطائف المعارف ص)

Hizi ni siku kumi za Dhul-hijjah. Hii ndio sahihi ambayo wapo juu yake jumhuri ya wenye kufasiri Qu-an, katika salafu na wengineo, na ndio kauli sahihi kutoka kwa Ibn ‘Abbās – Allāh amrishie[1]

Na Allāh kuapia kwa masiku haya ni dalili ya utukufu wa masiku haya, kama alivyosema As-suyutwi – Allāh amrehemu:

وَقَالَ أَبُو الْقَاسِمِ الْقُشَيْرِيُّ: الْقَسَمُ بِالشَّيْءِ لَا يَخْرُجُ عَنْ وَجْهَيْنِ إِمَّا لِفَضِيلَةٍ أَوْ لِمَنْفَعَةٍ فَالْفَضِيلَةُ كَقَوْلِهِ: ﴿ وَطُورِ سِينِينَ ۝٢ وَهَٰذَا ٱلْبَلَدِ ٱلْأَمِينِ ۝٣ ﴾ وَالْمَنْفَعَةُ نَحْوَ: ﴿ وَٱلتِّينِ وَٱلزَّيْتُونِ ﴾

Amesema Abul-Qaasim Al-Qushayry: Kiapo (cha Allāh) Kuapia kitu haitoki katika namna mbili, ima kwasababu ya ubora au manufaa. Ama (kuapia) kwa ubora kama kauli yake (Allāh), “Na ninaapa kwa Jabal Sinai. Na ninaapa kwa Mji huu Mtukufu”. Na (kuapia) kwa manufaa mfano, “Na ninaapa kwa mtini na mzaituni” [2]

2. Ni siku bora za Dunia

عَنْ جَابِرٍ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم، قَالَ: (أَفْضَلُ أَيَّامِ الدُّنْيَا أَيَّامُ الْعَشْرِ)

[1] Latwāiful-M’ārifu uk. 337

[2] Al-it-qaan Juzuu 4. Uk. 55

Kutoka kwa Jābir- Allāh amridhie, ya kwamba Mjumbe wa Allah ﷺ amesema, “Siku bora zaidi za Dunia ni Siku za kumi za mwezi wa Dhul-hijjah”[1]

3. Matendo ndani yake yana ujira mkubwa na yanapendeza zaidi kwa Allāh ﷻ

عَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ، قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم: (مَا مِنْ أَيَّامٍ الْعَمَلُ الصَّالِحُ فِيهَا أَحَبُّ إِلَى اللهِ عز وجل مِنْ هَذِهِ الْأَيَّامِ) يَعْنِي: أَيَّامَ الْعَشْرِ. قَالُوا: يَا رَسُولَ اللهِ، وَلا الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللهِ؟ قَالَ: (وَلا الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللهِ، إِلا رَجُلٌ خَرَجَ بِنَفْسِهِ وَمَالِهِ، ثُمَّ لَمْ يَرْجِعْ مِنْ ذَلِكَ بِشَيْءٍ)

Kutoka Kwa Ibn ‘Abbās – Allah amridhie- amesema: Amesema Mjumbe wa Allāh, ﷺ “ Hakuna katika siku ambazo matendo mema ndani yake yanapendeza zaidi kwa Allāh ﷻ kulikoni haya masiku” –anakusudia masiku kumi ya Dhul-hijjah. Wakasema Ewe Mjumbe wa Allāh! Hata jihadi katika njia ya Allāh? – wakakusudia nayo haifikii ujira wa masiku hayo kumi?. Akasema, “Hata jihadi katika njia ya Allāh; isipokuwa mtu ametoka mwenyewe na mali yake, kisha kisirejee chochote – yeye na mali yake”[2]

4. Ndio masiku matukufu na yanayopendeza mbele ya Allāh ﷻ

عَنْ ابْنِ عُمَرَ، عَنِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم، قَالَ: (مَا مِنْ أَيَّامٍ أَعْظَمُ عِنْدَ اللهِ وَلَا أَحَبُّ إِلَيْهِ الْعَمَلُ فِيهِنَّ مِنْ هَذِهِ الْأَيَّامِ الْعَشْرِ، فَأَكْثِرُوا فِيهِنَّ مِنَ التَّهْلِيلِ وَالتَّكْبِيرِ وَالتَّحْمِيد)

Kutoka kwa Ibnu ‘Umar, kutoka kwa Nabii ﷺ amesema, “Hakuna siku tukufu zaidi na zinazopendeza zaidi matendo ndani yake mbele ya Allāh kuliko siku kumi (za Dhul-hijjah). Basi fanyeni wingi wa Tahliil (Kusema: Lāilāha illa-llāhu), Takbiir (kusema: Allāhu Akbar), na Tahmiid (kusema: Alhamdulillah)”[3]

5. Siku ya Ijumā ndani ya Masiku kumi ni bora kuliko Ijumaa nyinginezo. Amesema Ibnu Hajar Al-‘asqlāniy – Allāh amrehemu:

ويوم الجمعة فيه أفضل من الجمعة في غيره لاجتماع الفضلين فيه

“Na siku ya Ijumā ndani yake ni bora zaidi kuliko Ijumā katika masiku mengine, kwa kukusanyika fadhila mbili ndani yake”[4]

6. Ndani yake hukusanyika ibada mama za uislamu. Amesema Ibnu Hajar Al-‘asqlāniy – Allāh amrehemu:

والذي يظهر أن السبب في امتياز عشر ذي الحجة لمكان اجتماع أمهات العبادة فيه، وهي الصلاة والصيام والصدقة والحج، ولا يتأتى ذلك في غيره

[1] Kash-fuli-Astaar Hadith na. 1128, ameisahihisha Sheikh Al-bāniy katika Swahihu At-targhiib wa At-tarhiib
[2] Musnad Ahmad Hadithi na. 1968
[3] Musnad Ahmad Hadithi na. 6154
[4] Fat-hul-bāry Juzuu 2 Uk. 460

“Na kile kinachodhihiri ni kwamba, sababu ya kuwa bora siku kumi za Dhul-Hijjah ni kuwa sehemu ya kukusanyika ibada mama ndani yake. Nazo ni: Swala, Swaumu, Swadaka, Hajj. Na wala halipatikani hilo katika masiku mengine”[1]

7. Masiku kumi ya mwanzo ya Dhul-hijja ni bora kulikoni masiku kumi ya Mwisho ya Ramadhani

والتحقيق ما قاله بعض أعيان المتأخرين من العلماء، أن يقال: مجموع هذا العشر أفضل من مجموع عشر رمضان، وإن كان في عشر رمضان ليلة لا يفضل عليها غيرها. والله أعلم

“Na uhakika ni kile walichokisema baadhi ya watu mashuhuri katika waliokuja baadae katika wanachuoni ya kwamba: Mkusanyiko wa kumi hili ni bora zaidi kuliko mkusanyiko wa kumi la mwisho la Ramadhani, na ijapokuwa katika kumi la Ramadhani kuna Lailatul-Qadr ambayo haufadhilishwi usiku mwingine dhidi yake. Na Allah ni mjuzi zaidi”[2]

8. Ni jumla ya masiku arobaini ambayo Allāh ﷻ alimuahidi Nabii Musa – Juu yake salamu. Anasema Allāh ﷻ

﴿ وَوَٰعَدۡنَا مُوسَىٰ ثَلَٰثِينَ لَيۡلَةٗ وَأَتۡمَمۡنَٰهَا بِعَشۡرٖ فَتَمَّ مِيقَٰتُ رَبِّهِۦٓ أَرۡبَعِينَ لَيۡلَةٗۚ ﴾ الأعراف [142]

“Na tulimuahidi Musa masiku thalathini na tukayakamilsha kwa masiku kumi, ikatimia miadi ya Mola Mlezi masiku arobaini” (Al-‘araaf, aya 142)

Akasema Imam Ibn Kathiir katika kuyabainisha hayo masiku arobaini:

وقد اختلف المفسرون في هذه العشر ما هي؟ فالأكثرون على أن الثلاثين هي ذو القعدة، والعشر عشر ذي الحجة. قاله مجاهد، ومسروق، وابن جريج. وروي عن ابن عباس. فعلى هذا يكون قد كمل الميقات يوم النحر، وحصل فيه التكليم لموسى، عليه السلام

“Kwa hakika wameofautiana watu wa tafsiir katika hili kumi, ni lipi hilo? Wengi wao wapo juu (ya kauli) ya kwamba; (siku) thalathini ni Mwezi wa Dhul-q’ida, na (siku) kumi ni za Mwezi wa Dhul-hijjah. Ameisema kauli hiyo: Mujāhid, Masruuq, Ibnu Jurayj, na imepokelewa kutoka kwa Ibnu ‘Abbās. Na juu ya kauli hii, anakuwa alikamilisha miadi siku ya kuchinja, na inakapatikana ndani yake (Allāh) kumzungumzisha Musa – Juu yake salamu”.[3]

9. Ndio masiku maalumu ambayo Allāh ﷻ ametaka watu wamtaje kwa wingi ndani yake

﴿ لِّيَشۡهَدُواْ مَنَٰفِعَ لَهُمۡ وَيَذۡكُرُواْ ٱسۡمَ ٱللَّهِ فِيٓ أَيَّامٖ مَّعۡلُومَٰتٍ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّنۢ بَهِيمَةِ ٱلۡأَنۡعَٰمِۖ فَكُلُواْ مِنۡهَا وَأَطۡعِمُواْ ٱلۡبَآئِسَ ٱلۡفَقِيرَ ٢٨ ﴾ الحج [28]

[1] Fat-hul-bāry Juzuu 2 Uk. 460
[2] Latwāiful-M’ārif Uk. 336
[3] Tafsiir Ibn Kathiir Juzuu 4 Uk. 468

“Ili washuhudie manufaa yao na walitaje jina la mola wako mlezi katika masiku maalum, juu ya kile Allāh alichowaneemesha katika wanyama hoa. Basi kuleni katika wanyama hao na mumlishe mwenye shida, aliye fakiri” (Al-hajj 28)

Amesema Imam Al-Baghawiy katika kuyabainisha hayo masiku maalumu:

وَيَذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ فِي أَيَّامٍ مَعْلُوماتٍ، يَعْنِي عَشْرَ ذِي الْحِجَّةِ فِي قَوْلِ أَكْثَرِ الْمُفَسِّرِينَ

“Na wataje jina la Allāh katika masiku maalumu, anakusudia masiku kumi ya Dhul-hijjah katika kauli ya wengi katika wafasiri”[1]

10.Kwa masiku haya hukhitimishwa Miezi Maalumu ya Hajji. Anasema Allāh ﷻ

﴿ ٱلۡحَجُّ أَشۡهُرٞ مَّعۡلُومَٰتٞۚ ﴾ البقرة [197]

“Hajji ni miezi maalum” (Al-baqara 197)

Akasema Imam Al-Baghawiy katika kubainisha hiyo miezi ya hajji

أَيْ: وَقْتُ الْحَجِّ أَشْهُرٌ مَعْلُومَاتٌ، وَهِيَ: شَوَّالٌ وَذُو الْقِعْدَةِ وَتِسْعٌ مِنْ ذِي الْحِجَّةِ إِلَى طُلُوعِ الْفَجْرِ مِنْ يَوْمِ النَّحْرِ، وَيُرْوَى عَنِ ابْنِ عُمَرَ: شَوَّالٌ وَذُو الْقِعْدَةِ وَعَشْرٌ مِنْ ذِي الْحِجَّةِ، وَكُلٌّ وَاحِدٍ مِنَ اللَّفْظَيْنِ صَحِيحٌ غير مختلف فيه، فَمَنْ قَالَ: عَشْرٌ عَبَّرَ بِهِ عَنِ اللَّيَالِي، وَمَنْ قَالَ تِسْعٌ عَبَّرَ بِهِ عَنِ الْأَيَّامِ، فَإِنَّ آخِرَ أَيَّامِهَا يَوْمُ عَرَفَةَ وَهُوَ اليوم التَّاسِعِ

“Anakusudia (Allāh) wakati wa Hajji ni miezi maalumu, ambayo ni: Shawwāl, Dhul-q’ada, na masiku tisa ya Dhul-hijjah mpaka kuchomoza kwa alfajiri siku ya kuchinja. Na imepokelewa kutoka kw Ibn ‘Umar: (Masiku hayo ni) Shawwāl, Dhul-q’ada na masiku kumi ya Dhul-hijjah. Na kila moja katika kauli mbili ni sahihi, hazitofautiani. Aliyesema: Kumi ameelezea kunako usiku, na aliyesema tisa, ameelezea kunako mchana, kwasababu mchana wa mwisho ni siku ya ‘Arafa nayo ni siku ya tisa”.[2]

MAANDALIZI KABLA YA KUINGIA MASIKU KUMI YA DHUL-HIJJAH

Yafuatayo ni baadhi ya mambo ambayo Muislam anatakiwa ayazingatie akiwa anaelekea katika masiku kumi matukufu ya Mwezi wa Dhul-hijjah

1. Kuihesabu nafsi kabla ya kuingia katika masiku haya matukufu

Ikiwa Muislam anayelekea masiku kumi matukufu ya Dhul-hijjah hana budi kuiandaa nafsi yake katika kufanya matendo mema. Ni misimu ambayo inakuja kwa nyakati maalum, hivyo Muislamu aone kuwa ni fursa kwake adhimu ya kuitumia katika maandalizi ya maisha yake ya baada ya haya maisha ya hapa Duniani. Na awe mtu anaona kuwa fursa hii huenda asiipate katika maisha yake kamwe. Basi mtu akumbuke Kauli ya Allāh ﷻ

[1] M’ālimu At-tanziil Juzuu 3 Uk.335
[2] M’ālimu At-tanziil Juzuu 1 Uk.250

﴿ حَتَّىٰٓ إِذَا جَآءَ أَحَدَهُمُ ٱلۡمَوۡتُ قَالَ رَبِّ ٱرۡجِعُونِ ٩٩ لَعَلِّيٓ أَعۡمَلُ صَٰلِحٗا فِيمَا تَرَكۡتُۚ كَلَّآۚ إِنَّهَا كَلِمَةٌ هُوَ قَآئِلُهَاۖ وَمِن وَرَآئِهِم بَرۡزَخٌ إِلَىٰ يَوۡمِ يُبۡعَثُونَ ١٠٠ ﴾ المؤمنون [99، 100]

“Mpaka mauti yatakapomuijia mmoja wao, atasema: Mola wangu nirejeshe. Ili niweze kufanya mema katika niliyoyaacha. (patasemwa): sivyo hivyo, hilo ni neno amelisema tu, na nyuma yao kuna kizuizi mpaka siku watakapofufuliwa” (Al-mu-uminuuna, Aya 99 - 100)

Na pia Kauli ya Allāh ﷻ katika hadithi Al-qudusy:

يَا عِبَادِي إِنَّمَا هِيَ أَعْمَالُكُمْ أُحْصِيهَا لَكُمْ ثُمَّ أُوَفِّيكُمْ إِيَّاهَا، فَمَنْ وَجَدَ خَيْرًا فَلْيَحْمَدِ اللهَ، وَمَنْ وَجَدَ غَيْرَ ذَلِكَ فَلَا يَلُومَنَّ إِلَّا نَفْسَهُ

Enyi waja wangu! Si vinginevyo haya (myatendao) ni matendo yenu nimeyadhibiti kwaajili yenu, kisha nitakupeni yote. Basi atakayekuta kheri amhimidi Allāh, na atakayekuta kinyume na hiyo (kheri) basi asiilaumu isipokuwa nafsi yake[1]

2. Kuomba dua unapoandama Mwezi wa Dhul-hijja

Ni Sunna unapoandama mwezi wa Dhul-hijjah au mwezi mwingineo wowote katika miezi ya Hijiria aombe dua iliyokuja katika hadithi:

عن بِلال بْن يَحْيَى بْنِ طَلْحَةَ بْنِ عُبَيْدِ اللهِ، عَنْ أَبِيهِ، عَنْ جَدِّهِ: أَنَّ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم كَانَ إِذَا رَأَى الْهِلالَ، قَالَ: (اللهُمَّ أَهِلَّهُ عَلَيْنَا بِالْيُمْنِ وَالْإِيمَانِ، وَالسَّلامَةِ وَالْإِسْلامِ، رَبِّي وَرَبُّكَ اللهُ)

Kutoka kwa Bilāl bin Yahya bin Twal-ha bin ‘Abdillah, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake, ya kwamba Mjumbe wa Allāh alikuwa akiona mwezi mwandamo anasema’ “Ewe Allah tudhihirishie mwezi kwa baraka, imani, salama na uislamu, mola wangu na mola wako ni Allāh”[2]

Dua kwa herufi za kiswahili:

Allāhumma! Ahillahu ‘alayna bil-yumni, wal-iimān, was-salāmati, wal-islām. Rabbii wa rabbuka llahu

MATENDO YANAYOFANYIKA KATIKA SIKU KUMI ZA DHUL-HIJJAH

1. Kumpwekesha Allāh ﷻ na kujiepusha na Shiriki

Tambua ewe ndugu! Tawhiid ni amali bora ambayo mtu atajikurubisha kwayo mbele ya Allāh ﷻ. Na Mtume wetu ﷺ amelitanabaisha hilo katika munasaba wa masiku hayo alipokuwa akielezea dua bora siku ya ‘Arafa akasema:

عَنْ طَلْحَةَ بْنِ عُبَيْدِ اللَّهِ ، أن رسول اللَّهِ صلى الله عليه وسلم، قَالَ: (أَفْضَلُ الدُّعَاءِ دُعَاءُ يَوْمِ عَرَفَةَ، وَأَفْضَلُ مَا قُلْتُ أَنَا وَالنَّبِيُّونَ مِنْ قَبْلِي: لا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَهُ)

[1] Sahiihu Muslim, Hadithi na. 2577
[2] Musnad Ahmad, Hadithi na. 1397

Kutoka kwa Twalha bin ‘Ubeydillah, yakwamba Mjumbe wa Allāh ﷺ amesema, “Bora zaidi ya dua siku ya ‘Arafa, na bora nilichokisema mimi na Manabii kabla yangu ni: Hapana muabudiwa wa haki isipokuwa Allāh pekee, asiye na mshirika”[1]

Mjumbe wa Allāh ﷺ anaonesha bora ya dua ni kusema: ***Lāilāha illa llahu wah-dahu la shariika lau***, ambapo neno hili huitwa neno la tawhiid, ni dalili ya kuwa bora ya matendo ya muislamu ya kumuweka karibu na Allāh ﷻ ni Tawhiid. Na pia ijulikane kinyume cha Tawhiid ni Shirki ambayo mtu akiifanya, matendo yake yote mema yanaharibika na kuwa ni katika waliopata hasara. Anasema Allāh ﷻ:

﴿وَلَقَدۡ أُوحِيَ إِلَيۡكَ وَإِلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكَ لَئِنۡ أَشۡرَكۡتَ لَيَحۡبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ ٱلۡخَٰسِرِينَ ٦٥﴾

الزمر [65]

Na kwa hakika umeteremshiwa wahyi na vilevile waliokuwa kabla yako ya kwamba, endapo ukifanya shirki, kwa hakika matendo yako yataharibika na utakuwa ni miongoni mwa waliopata hasara (Az-zumar, Aya 65)

Kama katika aya hii ameambiwa Mtukufu wa viumbe wa Allāh kuwa endapo akifanya shirki basi matendo yake yatabatilika, vipi mimi na wewe? Hivyo ni jukumu la kila Muislamu aijue shirki na kujiepusha nayo.

2. Funga ya Masiku tisa

Miongoni mwa matendo mema ya kufanya katika masiku haya kumi ni mtu kuyafunga haya masiku tisa, siku ya kumi ni ‘Eid ambapo hairuhusiwi kufunga. Amesema Mjumbe Allāh ﷺ:

(عَلَيْكَ بِالصَّوْمِ فَإِنَّهُ لَا مِثْلَ لَهُ)

“Lazimiana na funga, kwa hakika haina mfano wake”[2]

Imekuja katika hadithi ya Mama ‘Aisha kuwa Mtume hakuwahi kufunga swaumu ya masiku tisa.

عَنْ عَائِشَةَ رضي الله عنها قَالَتْ: مَا رَأَيْتُ رَسُولَ اللهِ صلى الله عليه وسلم صَائِمًا فِي الْعَشْرِ قَطُّ

Kutoka kwa ‘Aisha – Allah amridhie amesema: Sikuwahi kumuona Mjumbe wa Allāh katu akifunga masiku kumi (ya Dhul-hijjah)[3]

Na kutaja masiku kumi ni kwa makadirio na si kumi kwa ukamilifu wa idadi. Lakini imekuja hadithi nyingine kutoka kwa baadhi ya wakeze Mtume ﷺ kuthibitisha kuwa Mtume ﷺ alifunga masiku hayo kumi.

عَنْ بَعْضِ أَزْوَاجِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم قَالَتْ: كَانَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم يَصُومُ الْعَشْرَ وَثَلَاثَةَ أَيَّامٍ مِنْ كُلِّ شَهْرٍ؛ الِاثْنَيْنِ وَالْخَمِيسَ

[1] Al-Muwatwau, Hadithi na. 621
[2] Sunanu An-nasāi 2541
[3] Sahiihu Muslim, Hadithi na. 1176

Kutoka kwa baadhi ya wakeze ﷺ Nabii amesema: Alikuwa Nabii ﷺ anafunga masiku kumi (ya Dhul-hijjah), masiku matatu kila mwezi na siku ya Jumaatatu na Alhamisi[1]

Kauli yenye kukusanya hadhithi zenye kuthibitisha kufunga kwa Mtume ﷺ na zenye kupinga kufunga kwake

(i) Katika kanuni za Hadithi ni kuwa, hadithi inayothibitisha hutangulizwa na kufanyiwa kazi juu ya Hadithi inayopinga. Kwahyo itafanyiwa kazi hadithi yenye kuthibitisha funga ya Mtume ﷺ

(ii) Kanuni nyingine ni kuwa, mwenye ziada ya elimu hutangulizwa juu ya asiye na elimu. Hivyo itafanyiwa kazi hadithi yenye kuthibitisha funga ya Mtume ﷺ sababu kujua kuwa Mtume ﷺ alifunga ni elimu ya ziada juu ya asiyejua kuwa Mtume ﷺ alifunga

(iii) Inafahamika kuwa Siku ya Arafa imethibiti funga, basi inachukuliwa kuwa, Mama ‘Aisha – Allāh amridhie – anakusudia kuwa hakuwahi kumuona Mtume ﷺ akifunga kwa ukamilifu masiku yote tisa kwa ukamilifu.

Na mengineyo katika majibu waliyoleta wanachuoni katika kukusanya baina ya Hadithi hizo. Hivyo ni vyema Muislamu akatumia fursa ya masiku haya katika kufunga, sababu hadithi ilikuja kuonesha ubora wa matendo katika masiku haya kumi inaingia ndani yake swaumu, na Allāh ni mjuzi zaidi.

3. Hajji

Kama tulivyoona kuwa Hajji ina miezi maalum, na hukhitimishwa miezi hiyo kwa masiku haya kumi ya Dhul-hijjah. Matendo ya Hajji huanza siku ya nane, Siku ya Tarwiyah. Ikiwa Muislamu anawasaa wa kwenda kufanya hajji basi alifanye hilo. Hajji ya wajibu ni moja kwa maisha. Hivyo mtu kabla neema ya afya na uwezo kuondoka atumie fursa ya sasa ili akaitekeleze ibada hiyo adhimu.

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ. قَالَ: خَطَبَنَا رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم فقال (أَيُّهَا النَّاسُ! قَدْ فَرَضَ اللَّهُ عَلَيْكُمُ الْحَجَّ فَحُجُّوا " فقَالَ رَجُلٌ: أَكُلَّ عَامٍ؟ يَا رَسُولَ اللَّهِ! فَسَكَتَ. حَتَّى قَالَهَا ثَلَاثًا. فقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم" "لَوْ قُلْتُ: نَعَمْ. لَوَجَبَتْ. وَلَمَا اسْتَطَعْتُمْ)

Kutoka kwa Abuu Hurayra amesema: Alituhutubia sisi Mjumbe wa Allāh ﷺ akasema, “Enyi watu! Hakika Allāh amekuwajibishieni hajji, basi nendeni mkahiji”. Akasema mtu mmoja: Ewe Mjumbe wa Allāh! Ni kila mwaka?. Mtume akanyamaza. Mpaka mtu huyo aliposema mara tatu. Akasema Mjumbe wa Allāh ﷺ, “Lau ningesema ndio, basi ingekuwa wajibu – kuhiji kila mwaka – na msingeweza”

4. Kuchinja

Kuchinja ni miongoni mwa ibada bora za kujikurubisha kwa Allāh ﷻ ambapo mtu akiifanya na kuilekeza kwa asiye Allāh ﷻ mfano akiilekeza kwa Malaika, mizimu, majini,

[1] Sunanu An-naāi 2418

sharifu, mawalii n.k, basi inakuwa ni shiriki ambayo inamtoa mtu katika uislam na kubatilisha matendo yake. Anasema Allāh ﷻ:

﴿ قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦٢﴾ لَا شَرِيكَ لَهُ ۖ وَبِذَٰلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ ﴿١٦٣﴾ ﴾ الأنعام [162، 163]

“Sema (ewe Mtume): Hakika swala yangu, na kichinjwa changu, na uhai wangu, na kufa kwangu, vyote ni vya Mola Mlezi wa walimwengu wote. Hana mshirika, na hilo ndilo nimeamrishwa na mimi ni wa mwanzo katika Waislamu” (Al-an’ām, Aya 162 - 163)

5. **Kumtaja Allāh ﷻ**

Tumeona kuwa masiku haya kumi ndio masiku maalum ambayo mtu anatakiwa akithirishe adhkār ndani yake. Hivyo wakati wote mtu anatakiwa alete adhkār za aina mbalimbali tena kwa sauti kama walivyokuwa wakifanya Salafu. Amesema Imam Al-bukhār – Allāh amrehemu:

وَكَانَ ابْنُ عُمَرَ، وَأَبُو هُرَيْرَةَ: يَخْرُجَانِ إِلَى السُّوقِ فِي أَيَّامِ الْعَشْرِ، يُكَبِّرَانِ وَيُكَبِّرُ النَّاسُ بِتَكْبِيرِهِمَا. وَكَبَّرَ مُحَمَّدُ بْنُ عَلِيٍّ خَلْفَ النَّافِلَةِ

Alikuwa Ibnu ‘Umar na Abuu Hurayra – Allah awaridhie- wakienda sokoni katika masiku kumi ya Dhul-hijjah wanatoa takbiira, na watu wanatoa takbiira kwasababu ya takbiira zao. Na alitoa takbiira Muhammad bin ‘Ally mwishoni mwa sala za sunna[1]

6. **Kusoma Qur-an na vitabu vya sunna**

Kusoma Qur-an na vitabu vya sunna ni katika matendo mema, ndani yake kuna ujira wa kusoma, mtu anaongeza elimu na kuwaidhika kupitia maneno ya Allāh na Mtume wake. Anasema Ibnu Abii Ya’alā – Allāh amrehemu:

قَالَ مُهَنَّى: قلتُ لأَحْمَد بن حَنْبَلٍ: ما أَفْضَلُ الأعمال؟ قال: طَلَبُ العِلْمِ، قَالَ: لِمَنْ صَحَّتْ نِيَّتُهُ. قُلْتُ: وأَيْنِش تَصْحِيحُ النِّيَّة؟ قَالَ: يَنْوِي، يَتَواضَعُ فِيْهِ، ويَنْفِي عَنْه الجَهْلَ

Amesema Muhannā, “Nilisema kumuuliza Ahmad bin Hanbal: Ni lipi tendo bora zaidi katika matendo?”. Akasem: Kutafuta elimu, kwa yule itakayekuwa sahihi nia yake. Nikasema “Ni kwa lipi itakuwa sahihi nia?”. Akasema: Anuie kuwa mnyenyekevu katika kutafuta elimu na anajiondoshee ujinga[2]

7. **Kujibidiisha katika ibada za sunna**

Inatakikana Muislam kuchukua fursa ya masiku haya kufanya ibada mbalimbali za sunna, ikiwemo kuswali swala za sunna: Qabliyyah na Ba’adiyyah, Swala za Usiku, Swala ya Dhuhā, Sunna ya Udhu n.k, kutoa sadaka n.k. Hili litamfanya mtu apendwe zadi na Allāh. Anasema Allāh katika Hadiithul-qudusy:

وَمَا يَزَالُ عَبْدِي يَتَقَرَّبُ إِلَيَّ بِالنَّوَافِلِ حَتَّى أُحِبَّهُ، فَإِذَا أَحْبَبْتُهُ: كُنْتُ سَمْعَهُ الَّذِي يَسْمَعُ بِهِ، وَبَصَرَهُ الَّذِي يُبْصِرُ بِهِ، وَيَدَهُ الَّتِي يَبْطِشُ بِهَا، وَرِجْلَهُ الَّتِي يَمْشِي بِهَا، وَإِنْ سَأَلَنِي لَأُعْطِيَنَّهُ، وَلَئِنْ اسْتَعَاذَنِي لَأُعِيذَنَّهُ

[1] Sahiihul- bukhāry Juzuu 1 Uk. 339, Bābu fadhlil-‘amal fii Ayyāmil ‘Ashr
[2] Twabaqātul-hanābilah Juzuu 2 Uk. 476

“Na ataendelea mja kujikurubisha kwangu kwa sunna mpaka nitampenda. Nikisha mpenda nitakuwa sikio lake ambalo husikia kwako (yani hatosikiliza isipokuwa kinachomridhisha Allāh), na jicho lake ambalo hutumia kuonea (yani hatotazama isipokuwa kinachomridhisha Allāh), na mkono wake ambao hutumia kushikia (yani hatoshika sehemu ambayo Allāh haimridhishi), na mguu wake ambao hutumia kutembelea (yani hatokwenda na kukanyaga isipokuwa sehemu ambayo Allāh anairidhia). Na endapo akiniomba hakika nitampa, na endapo akiniomba kinga hakika nitamkinga”[1]

SIKU YA ARAFA

Fadhila za siku ya ‘Arafa

1. Ndio siku ambayo Allāh aliikamilisha dini yake

عَنْ عُمَرَ بْنِ الْخَطَّابِ، أَنَّ رَجُلًا مِنْ الْيَهُودِ قَالَ لَهُ:يَا أَمِيرَ الْمُؤْمِنِينَ، آيَةٌ فِي كِتَابِكُمْ تقرؤونها، لَوْ عَلَيْنَا مَعْشَرَ الْيَهُودِ نَزَلَتْ لَاتَّخَذْنَا ذَلِكَ الْيَوْمَ عِيدًا. قَالَ: أَيُّ آيَةٍ؟ قَالَ: {الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الإِسْلامَ دِينًا}. قَالَ عُمَرُ: قَدْ عَرَفْنَا ذَلِكَ الْيَوْمَ، وَالْمَكَانَ الَّذِي نَزَلَتْ فِيهِ عَلَى النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم، وَهُوَ قَائِمٌ بِعَرَفَةَ يَوْمَ جُمُعَةٍ

Kutoka kwa ‘Umar bin Khatwāb; ya kwamba mtu mmoja alisema kumwambia: Ewe Amiri wa Waumini! Kuna aya katika kitabu chenu mnaisoma, lau ingeteremka kwetu mayahudi tungeifanya siku hiyo iwe ni ‘Eid. Akasema (‘Umar): Ni aya ipi? Akasema, “Leo nimekukamilishieni dini yenu, na nimekutimizieani neema zangu kwenu, na nimeridhia Uislamu ndio uwe dini yenu” (Al-māidah aya 3). Akasema ‘Umar: kwa hakika tunaijua siku hiyo, na sehemu ambayo Aya hiyo imeteremka kwa Nabii ﷺ, na yeye amesimama ‘Arafa, Siku ya Ijumā.[2]

2. Allāh huwaacha huru kutokana na Moto wengi katika waja wake
3. Allāh hujifakharisha kwa waja wake mbele ya Malaika

قَالَتْ عَائِشَةُ : إِنَّ رَسُولَ اللهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ: (مَا مِنْ يَوْمٍ أَكْثَرَ مِنْ أَنْ يُعْتِقَ اللهُ فِيهِ عَبْدًا مِنَ النَّارِ مِنْ يَوْمِ عَرَفَةَ، وَإِنَّهُ لَيَدْنُو، ثُمَّ يُبَاهِي بِهِمُ الْمَلَائِكَةَ، فَيَقُولُ: مَا أَرَادَ هَؤُلَاءِ)

Amesema ‘Aisha – Allāh amridhie- ya kwamba Mjumbe wa Allāh ﷺ amesema, “Hakuna katika siku Allāh hukihirisha kuwaachia huru waja kutokana na moto kulikoni siku ya ‘Arafa, na kwamba yeye anakurubia (ukurubiaji unaolingana na utukufu wake), kisha anajifakhari kwa Malaika anasema: Ni nini wanataka hawa?”[3]

4. Funga yake ni kafara ya madhambi ya miaka miwili. Amesema Mjumbe wa Allāh ﷺ

صِيَامُ يَوْمِ عَرَفَةَ أَحْتَسِبُ عَلَى اللهِ أَنْ يُكَفِّرَ السَّنَةَ الَّتِي قَبْلَهُ، وَالسَّنَةَ الَّتِي بَعْدَهُ

[1] Sahiihul- bukhāry, Hadithi na. 6137
[2] Sahiihul- bukhāry, Hadithi na. 45
[3] Sahiihu Muslim, Hadithi na. 1348

"Kufunga Siku ya ‘Arafa, ninaihesabu mbele ya Allāh ni kufutio cha madhambi ya mwaka uliopita na mwaka ujao”[1]

Ibada zinazofanywa siku ya ‘Arafa

1. Funga

Kama hadithi iliyotangulia katika kuelezea swaumu ya Siku ya ‘Arafa kuwa ni kafara ya madhambi ya miaka miwili, hivyo muislamu anahimizwa kufunga siku hii, hasa ikiwa ameshindwa kufunga masiku mengineyo kabla yake. Ama mtu akiwa katika ibada ya hajji yeye si sunna kwake kufunga siku hii, na kufungua kwake ni bora zaidi, kama ambavyo Mtume wa Allāh ﷺ hakufunga ‘Arafa akiwa ni mwenye kufanya hajji.

2. Kukithirisha dua na dhikri

Siku hii ya ‘Arafa mtu anahimizwa kuomba dua na kufanya adhkār, kuanzia alfajiri yake. Na zaidi ni kuleta takbiira mpaka siku ya mwisho ya Masiku ya Tashriiq. Na bora ya kile atakachokisema ni neno la tawhiid.

عَنْ طَلْحَةَ بْنِ عُبَيْدِ اللَّهِ ، أن رسول اللَّهِ صلى الله عليه وسلم، قَالَ: (أَفْضَلُ الدُّعَاءِ دُعَاءُ يَوْمِ عَرَفَةَ، وَأَفْضَلُ مَا قُلْتُ أَنَا وَالنَّبِيُّونَ مِنْ قَبْلِي: لا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَهُ)

Kutoka kwa Twalha bin ‘Ubeydillah, yakwamba Mjumbe wa Allāh ﷺ amesema, “Bora zaidi ya dua siku ya ‘Arafa, na bora nilichokisema mimi na Manabii kabla yangu ni: Hapana muabudiwa wa haki isipokuwa Allāh pekee, asiye na mshirika”[2]

3. Mahujaji kusimama katika viwanja vya ‘Arafāt

عن عَبْد الرَّحْمَنِ بْن يَعْمَرَ الدِّيلِيّ يَقُولُ: شَهِدْتُ رَسُولَ اللهِ صلى الله عليه وسلم وَهُوَ وَاقِفٌ بِعَرَفَةَ وَأَتَاهُ نَاسٌ مِنْ أَهْلِ نَجْدٍ، فَقَالُوا: يَا رَسُولَ اللهِ، كَيْفَ الْحَجُّ؟ فَقَالَ: " الْحَجُّ عَرَفَةُ، فَمَنْ جَاءَ قَبْلَ صَلَاةِ الْفَجْرِ مِنْ لَيْلَةِ جَمْعٍ، فَقَدْ تَمَّ حَجُّهُ

Kutoka kwa ‘Abdirrahman bin Ya’amar Ad-diyly amesema: Nilimshuhudia Mjumbe wa Allāh ilihali amesimama ‘Arafa, na wakamuijia yeye watu, katika watu wa Najdi wakasema: Ewe Mjumbe wa Allah! Ni vipi huwa hajji? Akasema, “Hajji ni kusimama ‘Arafa, atakayekuja (‘Arafa) kabla ya swala ya Alfajiri ya Usiku wa Muzdalifa (Usiku wa ‘Eid), basi hajji yake itakuwa imetimia”[3]

SIKU YA ‘EIDUL-ADH-HA

Fadhila za Siku ya ‘Eidul-adh-ha

Siku hii ni siku tukufu zaidi katika masiku mbele ya Allāh ﷻ

عَنْ عَبْدِ اللهِ بْنِ قُرْطٍ أَنَّ رَسُولَ اللهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ: " أَعْظَمُ الْأَيَّامِ عِنْدَ اللهِ يَوْمُ النَّحْرِ، ثُمَّ يَوْمُ الْقَرِّ

[1] Sahiihu Muslim, Hadithi na. 1162
[2] Al-Muwatwau, Hadithi na. 621
[3] Musnad Ahmad, Hadithi na. 18774

Kutoka kwa Abdullah bin Qur-twiy, ya kwamba Mjumbe wa Allāh amesema, “Siku tukufu zaidi katika masiku mbele ya Allāh ni siku ya kuchinja, kisha siku ya Al-qarr (Mwezi kumi na moja)”[1]

Ibada ndani ya Siku ya ‘Eidul-adh-ha

1. Kuchinja

Yule ambaye Allāh amempa wasaa basi achinje siku ya ‘Eidul-Adh-hā, au masiku mawili baada yake.

Hukumu ya Udh-hiya

Wanachuoni wametofautiana juu ya hukmu ya Udh-hiya. Lakini kauli yenye nguvu ni kuwa ni wajibu kwa mwenye uwezo, kwasababu ya matamko ya hadithi

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ: أَنَّ رَسُولَ اللهِ صلى الله عليه وسلم قَالَ: "مَنْ كَانَ لَهُ سَعَةٌ وَلَمْ يُضَحِّ، فَلَا يَقْرَبَنَّ مُصَلَّانَا

Kutoka kwa Abuu Hurayra ya kwmba Mjumbe wa Allāh ﷺ amesema, “Yule ambaye atakayekuwa na wasaa na hakuchinja, basi asiukaribie muswala wetu wa ‘Eid”[2]

Mambo ya kujiepusha kwa mwenye kusudia kuchinja unapoandama mwezi wa Dhul-hijjah.

Amesema Mjumbe wa Allāh ﷺ:

إِذَا دَخَلَتِ الْعَشْرُ، فَأَرَادَ رَجُلٌ أَنْ يُضَحِّيَ، فَلَا يَمَسَّ مِنْ شَعْرِهِ، وَلَا مِنْ بَشَرِهِ

“Pindi litakapoingia kumi (la mwanzo la Dhul-hijjah) na akataka mmoja wenu kuchinja, basi asiguse nywele zake na katika ngozi zake”[3]

Vilevile imekuja riwaya nyingineyo, Amesema Mjumbe wa Allāh ﷺ:

مَنْ كَانَ لَهُ ذِبْحٌ يَذْبَحُهُ،فَإِذَا أُهِلَّ هِلَالُ ذِي الْحِجَّةِ، فَلَا يَأْخُذَنَّ مِنْ شَعْرِهِ وَلَا مِنْ أَظْفَارِهِ شَيْئًا حَتَّى يُضَحِّيَ

“Yeyote mwenye kichinjwa cha kumchinja, pindi utakapoandama mwezi wa Dhul-hijjah, basi asichukue katika nywele zake, wala katika kucha zake chochote mpaka atakapochinja”[4]

Hivyo kulingana na Hadithi hizi mbili, inatakiwa mwenye nia ya kuchinja, pindi utakapoigia mwezi wa Dhul-hijjah basi asinyoe nywele zake, kukata kucha zake na kutoa sehemu katika ngozi yake.

Makatazo hayo ni ya kuharamisha, kwa maana atakayefanya katika hayo makatazo anapata dhambi ila hana kafara, na Udh-hiya wake atafaa kumchinja. Amesema Ibnu Qudāmah – Allāh amrehemu

وَمُقْتَضَى النَّهْيِ التَّحْرِيمُ

“Na muktadha wa makatazo ni kuharamisha”[5]

[1] Sunanu Abii Dāud, Hadithi na. 1765
[2] Sunanu Ibn Mājah, Hadithi na. 3123
[3] Musnad Ahmad, Hadithi na. 26474
[4] Sahiihu Muslim, Hadithi na. 1977
[5] Al-mughniy, Juzuu 13 Uk. 362 - 363

فإنَّه يترُكُ قَطْعَ الشَّعَرِ وتَقْلِيمَ الأظفارِ، فإنْ فَعَلَ اسْتَغْفَرَ اللَّه تعالَى. ولا فِدْيَةَ فيه إجْماعًا، سواءٌ فَعَلَه عَمْدًا أو نِسْيانًا

"Basi inatakikana kwake kuacha kukata nywele na kucha. Endapo akilifanya hilo (la kukata nywele na kucha), atamuomba Allāh msamaha, na hana fidia katika hilo kwa makubaliano ya wanachuoni, sawasawa amefanya kwa makusudi au kuwa kusahau"[1]

Endapo ikitokea haja ya kukata nywele, kucha au sehemu katika ngozi basi hatopata dhambi, kamavile; kupata adha na madhara kwa kuacha nywele au kucha, au kupata maumivu makali basi atazikata kwa kadri ya haja, kulingana na kanuni isemayo:

الضرورات تبيح المظورات

Dharura huhalalisha yaliyokatazwa

<u>Hekima ya makatazo ya kuchukua sehemu katika kucha, nywele au ngozi</u>

Amesema Imām An-nawawiy – Allāh amrehemu:

قَالَ أَصْحَابُنَا وَالْحِكْمَةُ فِي النَّهْيِ أَنْ يَبْقَى كَامِلَ الْأَجْزَاءِ لِيُعْتِقَ مِنَ النَّارِ وَقِيلَ التَّشَبُّهُ بِالْمُحْرِمِ قَالَ أَصْحَابُنَا هذا غلط لأنه لايعتزل النساء ولايترك الطِّيبَ وَاللِّبَاسَ وَغَيْرَ ذَلِكَ مِمَّا يَتْرُكُهُ الْمُحْرِمُ

Wamesema watu wa madhehebu yetu, na hikma katika makatazo ni, abakie mtu mkamilifu wa sehemu zake ili aweze kuachwa huru na moto. Na pamesemwa: (Hekima) ni yeye kushabihiana na muhrimu (aliye nuia na akaingia katika hajji au umra). Wakasema watu wa madhehebu yetu: hili ni kosa, sababu yeye hajitengi na wanawake, na wala haachi manukato na nguo (zilizoshonwa) na mengineyo katika yale ayaachayo muhrimu.[2]

<u>Kuchinja Udh-hiya ni bora kuliko kutoa sadaka ya thamani yake</u>

Amesema Imām Ibn Qudāmah Al-Maqdisy – Allāh amrehemu:

وذبحها أفضل من الصدقة بثمنها

"Na kuchinja udh-hiya ni bora zaidi kulikoni kutoa sadaka kwa thamani (pesa) yake"[3]

<u>Muda wa kuchinja Udh-hiyah</u>

Amesema Imām Ibn Qudāmah Al-Maqdisy – Allāh amrehemu:

أمَّا أوَّلُه، فظاهِرُ كلامِ الخِرَقِيّ أنَّه إذا مَضَى من نهارِ يومِ العيدِ قَدْر تَحُلُّ فيه الصلاةُ، وقَدْرُ الصَّلاةِ والخُطْبَتَيْنِ تامَّتَيْنِ فى أخَفِّ ما يكون، فقد دَخَلَ وَقْتُ الذَّبْحِ، ولا يُعْتبَرُ نفسُ الصلاةِ، لا فَرْقَ فى هذا بينَ أهلِ المِصْرِ وغيرِهم. وهذا مذهبُ الشافِعِيّ، وابنِ المُنذِرِ. وظاهِرُ كلامِ أحمد

Muda wa mwanzo wake, dhahiri ya maneno ya Al-khiraqy ni kwamba, utakapopita katika sehemu ya mchana siku ya 'Eid makadirio ya kuingia swala, na makadirio ya swala na khutba mbili kwa ukamilifu wake kwa wepesi

[1] Al-mughniy, Juzuu 13 Uk. 363
[2] Sharhu An-nawawiy 'alā sahiih Muslim, Juzuu 13 Uk,139
[3] Al-mughniy Juzuu 13 Uk. 134

uwezekanao, basi utakua umeingia wakati wa kuchinja. Na wala haizingatiwi ile swala yenyewe. Hakuna utofauti katika hili baina ya watu mjini na wengineo. Na hii ndio madhehebu ya Imām Shāfy, na Ibn Mundhiri, na dhahiri ya maneno ya Imām Ahmad[1]

وآخِرُه آخِرُ اليومِ الثانِي من أيامِ التَّشْرِيقِ، فتكونُ أيامُ النَّحْرِ ثلاثةً؛ يومُ النَّحْرِ ويَوْمان بَعْدَه

“Na muda wa mwisho ni siku ya pili ya Masiku ya Tashriiq. Inakuwa masiku ya kuchinja ni matatu, siku ya kuchinja (‘Eid) na masiku mawili baadae”[2]

Kwa ufupi ni kuwa, muda wa mwazo kuanza kuchinja ni siku ya ‘Eidul-adh-ha kwa kukadiria kutoka muda wa makatazo, ambapo jua likichomoza mpaka kunyanyuka makadirio ya mkuki, kisha akadirie muda wa swala ya rakā mbili hafifu lakini yenye kutimia, kisha makadirio ya muda wa khutba, yani anaweza kukadiria dakika 10 za swala, na dakika 20 za khutba kisha akaanza kuchinja mnyama wake – Allāh ni mjuzi zaidi. Sawasawa iwe ni sehemu ambayo huswaliwa swala ya ‘Eid au haiswaliwi, kama sehemu za mashambani n.k. Na muda wa mwisho unakuwa siku ya pili ya Siku za Tashriiq kabla ya kuingia magharibi

<u>Bora katika kichinjwa cha Udh-hiya</u>

Ikiwa Muislamu anahiyari ya kuchinja aina kadhaa ya wanyama hoa, basi inabidi afuate utaratibu katika kuchagua mnyama bora zaidi. Amesema Imām Ibn Qudāmah Al-Maqdisy – Allāh amrehemu:

والأفضل فيها الإبل ثم البقر ثم الغنم. والذكر والأنثى سواء

“Na bora zaidi katika (wanyama hoa) ni ngamia, kisha ng’ombe, kisha mbuzi na kondoo. Dume na jike ni sawasawa”[3]

Na ikiwa una aina moja ya wanyama wa kuchinja, bora zaidi katika sifa ni mnene zaidi, mwenye nyama nyingi, mwenye umbile kamili zaidi na muonekano mzuri.

عن أَنَس بْن مَالِكٍ قَالَ: كَانَ رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم يُضَحِّي بِكَبْشَيْنِ أَقْرَنَيْنِ أَمْلَحَيْنِ، وَكَانَ يُسَمِّي وَيُكَبِّرُ، وَلَقَدْ رَأَيْتُهُ يَذْبَحُهُمَا بِيَدِهِ وَاضِعًا عَلَى صِفَاحِهِمَا قَدَمَهُ

Kutoka kwa Anas bin Māliki amesema: Alikuwa Mjumbe wa Allāh anachinja kondoo mkubwa, mwenye pembe, mwenye rangi nyeupe ilichanganyika na weusi. Na alikuwa anamtaja Allāh na kumkabiri. Na hakika nilimuona akiwachinja kwa mikono yake, akiwa ameweka mguu wake juu ya ubavu wa kondoo[4]

[1] Al-mughniy, Juzuu 13 Uk. 384
[2] Al-mughniy, Juzuu 13 Uk. 386
[3] Al-muqni’u Uk. 132
[4] Musnad Ahmad, Hadithi na. 11960

Masharti ya mnyama wa Udh-hiya

(i) Awe ni katika wanyama hoa: Mbuzi, kondoo, ng'ombe na ngamia. Anasema Allāh ﷻ:

﴿ وَلِكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنسَكًا لِّيَذْكُرُواْ ٱسْمَ ٱللَّهِ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّنۢ بَهِيمَةِ ٱلْأَنْعَٰمِ ﴾ الحج [34]

Na Kila umma tumewafanyia sehemu ya kuchinja mnyama, ili waweze kutaja jina la Allāh kwa kile alichowaruzuku katika wanyama hoa (Al-hajj, Aya 34)

(ii) Afikie umri uliwekwa katika sheria: Mbuzi awe na mwaka mmoja na zaidi, kondoo miezi sita na zaidi, ng'ombe miaka miwili na zaidi na ngamia miaka mitano na zaidi

عَنْ جَابِرٍ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم: (لَا تَذْبَحُوا إِلَّا مُسِنَّةً، إِلَّا أَنْ يَعْسُرَ عَلَيْكُمْ فَتَذْبَحُوا جَذَعَةً مِنَ الضَّأْنِ)

Kutoka kwa Jābir Amesema: Amesema Mjumbe wa Allāh ﷺ, "Msichinje isipokuwa ngamia mwenye miaka mitano au ng'ombe mwenye miaka miwili au mbuzi wa mwaka mmoja, isipokuwa kukiwa na uzito kwenu, basi chinjeni kondoo aliyetimiza miezi sita"[1]

(iii) Aepukane na dosari yenye kupelekea kutofaa kuchinjwa kwaajili ya udh-hiya. Na dosari zenyewe ni chongo ya wazi, maradhi ya wazi, kilema cha wazi na kuvunjika kiungo

سَمِعْتُ عُبَيْدَ بْنَ فَيْرُوزَ مَوْلَى بَنِي شَيْبَانَ أَنَّهُ سَأَلَ الْبَرَاءَ عَنِ الْأَضَاحِيِّ، مَا نَهَى عَنْهُ رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم وَمَا كَرِهَ، فَقَالَ: قَالَ رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم أَوْ قَامَ فِينَا رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم وَيَدِي أَقْصَرُ مِنْ يَدِهِ، فَقَالَ: (أَرْبَعٌ لَا تُجْزِئُ: الْعَوْرَاءُ الْبَيِّنُ عَوَرُهَا، وَالْمَرِيضَةُ الْبَيِّنُ مَرَضُهَا، وَالْعَرْجَاءُ الْبَيِّنُ ظَلْعُهَا، وَالْكَسِيرُ الَّتِي لَا تُنْقِي)

Nilimsikia 'Ubayd bin Fayruuz, Mtwana wa banii Shaybaan, kwamba yeye alimuuliza Al-baraa kunako vichinjwa vya Udh-hiya ambavyo Mjumbe wa Allāh amevikataza, na vinavyochukiza kuchinjwa. Akasema: Amesema Mjumbe wa Allāh ﷺ au alisimama baina yetu Mjumbe wa Allāh na mkono wangu ni mfupi kuliko wake akasema, "Aina nne ya wanyama hawafai: Chongo ambaye chongo yake ipo wazi, na mgonjwa ambaye maradhi yake yapo wazi, na kilema ambaye kilema chake kipo wazi, na aliyevunjika ambaye mfupa wake hauna uboho"[2]

(iv) Awe mwenye kuchinja ana umiliki kamili au awe amepewa idhini na sheria au mmiliki. Hivyo itafaa kuchinja katika mnyama wa yatima akiwa anapenda hilo, au kuwa wakala wa kuchinja kwa idhini ya mmiliki

(v) Asifungamane mnyama huyo na haki ya mtu mwingine. Haitofaa kuchinja mnyama aliyewekwa rehani

(vi) Awe amechinjwa katika wakati uliowekwa katika sheria

[1] Sahiihu Muslim, Hadithi na. 1963
[2] Musnad Ahmad, Hadithi na. 18510

Wanyama walio makruhu kuchinjwa

Wanyama Makruhu kuchinjwa ni wale ambao sio bora ki-sifa kuchinjwa, japokuwa watafaa kuchinjwa kukiwa hakuna wengine bora zaidi yao. Sifa za wanyama hao ni:

(i) Aliyekatika nusu au zaidi ya pembe au sikio
(ii) Aliyekatwa sikio kwa upana kuaniza mbele au kuanzia nyuma
(iii) Aliyeondoshwa sikio lote
(iv) Aliyeondoshwa pembe lote - siye ambaye hana asili ya pembe
(v) Aliyepigwa kwenye jicho na akawa kipofu pasi na kuondosha jicho
(vi) Asiyeweza kufuata kundi la mbuzi au kondoo kwa udhaifu alionao mpaka asindikizwe kwa kumuongoza mpaka afikie kundi au anakaa nyuma ya kundi kwa udhaifu
(vii) Aliyekatwa nusu ya mkia wake
(viii) Ambaye meno yake yamedondoka kwa umri mkubwa
(ix) Aliyekatwa sehemu ya vyenye kubebea chuchu

Kipi kinachotosheleza katika kichinjwa?

Mtu mmoja inatosha kuchinja mbuzi au kondoo mmoja kwajili yake na watu wa nyumba yake. Na inatosheleza kushirikiana watu saba katika ng'ombe au ngamia

عن عَطاءَ بن يَسارٍقال:سَأَلْتُ أبا أيُّوبَ: كَيْفَ كانَتِ الضَّحايا على عَهْدِ رَسولِ اللهِ صلى الله عليه وسلم؟ فقال: كانَ الرَّجُلُ يُضَحِّي بالشَّاةِ عَنْهُ وعن أهْلِ بَيْتِهِ، فيأْكُلُونَ وَيُطْعِمُونَ

Kutoka kwa 'Atwā bin Yasār anasema: Nilimuuliza Abuu Ayyuub: vipi ilikuwa vichinjwa katika zama za Mtume ﷺ? Akasema: ilikuwa Mtu anachinja mbuzi kwaajili yake na watu wa nyumba yake, wanamla na kutoa sadaka[1]

Kutoka kwa 'Aliy – Allāh amridhie amesema:

فَأَمَرَنَا رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم أَنْ نَشْتَرِكَ فِي الْإِبِلِ وَالْبَقَرِ، كُلُّ سَبْعَةٍ مِنَّا فِي بَدَنَةٍ

"Ametuamrisha sisi Mjumbe wa Allāh tushirikiane katika ngamia na ng'ombe, kila watu saba katika ng'ombe au ngamia mmoja"[2]

Nini aseme wakati wa kuchinja?

Amesema Imām Ibn Qudāmah Al-Maqdisy – Allāh amrehemu:

ثَبَتَ أنّ النَّبِيَّ صلى الله عليه وسلم كان إذا ذَبَحَ قال: "بِسْمِ اللهِ، واللهُ أكْبَرُ" وفى حديثِ أنَسٍ: وسَمَّى وكبَّرَ وكذلك كان يقول ابنُ عمرَ. وبه يقولُ أصحابُ الرَّأْيِ، ولا نَعْلَمُ فى اسْتِحْبابِ هذا خِلافًا، ولا فى أنَّ التَّسْمِيَةَ مُجْزِئَةٌ. وإنْ نَسِيَ التَّسْمِيَةَ، أجْزَأَه، على ما ذكرنا فى الذَّبائحِ. وإنْ زادَ فقال: اللهُمّ هذا مِنْكَ ولَكَ، اللهُمّ تَقَبَّلْ مِنِّى، أو مِنْ فلانٍ. فحَسَنٌ. وبه قال أكثرُ أهلِ العِلْمِ

"Imethibiti ya kwamba Nabii ﷺ alipokuwa akichinja anasema "kwa jina la Allāh, Allāh ni mkubwa". Na katika hadithi ya Anas: Na alimtaja Allāh, na kumkabiri, hivyo hivyo alikuwa akisema Ibn 'Umar. Na kwa kauli hiyo ndio wamesema watu

[1] Jāmi'u Attirmidhy, Hadithi na. 1582
[2] Sahiihu Muslim, Hadithi na. 1213

wa rai. Na hatujui khilafu ya hilo kuwa ni mustahabu, na ya kwamba kusema 'Bismillah' kuwa inatosheleza. Na endapo akisau kusema 'Bismillah' kitafaa kichinjwa, kwa kile tulishokitaja katika vichinjwa. Na endapo akizidisha akasema: Ewe Allāh! hiki kimetoka kwako na kwaajili yako, ewe Allāh! Nikubalie mimi na mkubalie fulani basi ni vyema, na kwahilo wamesema wanachuoni"[1]

Dua kwa maandishi ya kiswali
Bismillah, Allāhu Akbar, Allāhumma hādha minka wa laka, Allāhumma taqabbal minnii

<u>Namna ya kugawanya nyama ya Udh-hiya</u>
Amesema Allāh ﷻ:

﴿لِّيَشۡهَدُواْ مَنَٰفِعَ لَهُمۡ وَيَذۡكُرُواْ ٱسۡمَ ٱللَّهِ فِيٓ أَيَّامٖ مَّعۡلُومَٰتٍ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّنۢ بَهِيمَةِ ٱلۡأَنۡعَٰمِۖ فَكُلُواْ مِنۡهَا وَأَطۡعِمُواْ ٱلۡبَآئِسَ ٱلۡفَقِيرَ ٢٨﴾ الحج [28]

Ili waweze kushuhudia manufaa yao na walitaje jina la Allāh katika masiku maalum juu ya kile alichowaneemesha katika wanyama hoa. Basi kuleni katika wanyama hao na mumlishe mwenye shida, fakiri (Al-hajj 28)

Amesema Imām Ibn Qudāmah Al-Maqdisy – Allāh amrehemu:

قال أَحْمَدُ: نحنُ نَذْهَبُ إلى حديثِ عبدِ اللَّه: يَأْكُلُ هو الثلُثَ، ويُطْعِمُ مَنْ أرادَ الثُّلُثَ، ويَتَصَدَّقُ على المساكِينِ بالثُّلُثِ. قال عَلْقَمَةُ: بَعَثَ مَعِى عبدُ اللَّهِ بِهَدِيَّة، فأَمَرَنِى أن آكُلَ ثُلُثًا، وأن أُرْسِلَ إلى أهلِ أخِيهِ بثُلُثٍ، وأَنْ أَتَصَدَّقَ بثُلُثٍ. وعن ابنِ عمرَ قال: الضَّحايَا والهَدايَا ثُلُث لَكَ، وثُلُث لأَهْلِكَ، وثُلُثٌ للمساكِين. وهذا قولُ إسحاقَ، وأحَدُ قَوْلَى الشافِعِى. وقال فى الآخرِ: يَجْعَلُها نِصْفَيْنِ، يَأْكُلُ نِصْفًا، ويَتَصَدَّقُ بنِصْفٍ

Amesema Ahmad: Sisi tunakwenda katika hadithi ya 'Abdillah: Anakula theluthi, na analisha theluthi mwenye kutaka, Na anatoa sadaka theluthi kwa masikini. Amesema 'Alqamah: Alinituma 'Abdullah nipeleke zawadi, akaniambia nile theluthi, na nipeleke theluthi kwa watu wa kaka yake, na nitoe sadaka theluthi. Na kutoka kwa Ibn Umara amesema: Kichinjwa cha Udh-hiya na Hady, theluthi yako, theluthi ya ahli zako, na theluthi ya masikini. Na hii ndio kauli ya Is-hāq, na moja katika kauli za Shāfy. Na akasema (Imam Shāfy): Atafanya nyama nusu mbili, anakula nusu na anatoa sadaka nusu[2]

Kwaujumla ni bora aweke mafungu matatu: theluthi yake na familia yake, theluthi anawalisha wenye shida, na theluthi anatoa sadaka. Na pia anaweza kutoa sehemu aitakayo sadaka na nyingine atakula yeye na familia yake

[1] Almughniy, Juzuu Juzuu 13 Uk.390
[2] Almughniy, Juzuu Juzuu 13 Uk.379

2. Kuswali Swala ya ‘Eidul-adh-ha

Baadhi ya adabu ya siku ya Eidul-adh-ha

(a) Kupendeza na kuvaa nguo nzuri

عَنْ سَالِمٍ ، عَنْ أَبِيهِ قَالَ: وَجَدَ عُمَرُ بْنُ الْخَطَّابِ رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُ حُلَّةً مِنْ إِسْتَبْرَقٍ بِالسُّوقِ، فَأَخَذَهَا فَأَتَى بِهَا رَسُولَ اللهِ صلى الله عليه وسلم فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللهِ ابْتَعْ هَذِهِ فَتَجَمَّلْ بِهَا لِلْعِيدِ وَالْوَفْدِ، فَقَالَ رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم: إِنَّمَا هَذِهِ لِبَاسُ مَنْ لَا خَلَاقَ لَهُ أَوْ: إِنَّمَا يَلْبَسُ هَذِهِ مَنْ لَا خَلَاقَ لَهُ

Kutoka kwa Sālimu, kutoka kwa baba yake amesema: Alipata ‘Umar bin Al-khatwāb – Allāh amridhie- nguo iliyotengenezwa kwa hariri kutoka sokoni, akaichukua na akamuendea nayo Mjumbe wa Allāh ﷺ akasema: Ewe Mjumbe wa Allāh inunue hii nguo na ujipambe kwayo kwenye ‘Eid na wageni. Akasema Mjumbe wa Allāh ﷺ: Hakika hili ni vazi la wasio na hadhi au alisema si vinginevyo, hulivaa vazi hili asiye na hadhi[1]

Hapa katika hadithi hii Mtume ﷺ alipinga kuvaa hariri ila akakubali kujipamba kwaajili ya ‘Eid

(b) Kutokula chochote wakati wa kwenda kuswali

عَبْدُ اللهِ بْنُ بُرَيْدَةَ، عَنْ أَبِيهِ، قَالَ: كَانَ رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم لَا يَغْدُو يَوْمَ الْفِطْرِ حَتَّى يَأْكُلَ، وَلَا يَأْكُلُ يَوْمَ الْأَضْحَى حَتَّى يَرْجِعَ، فَيَأْكُلَ مِنْ أُضْحِيَّتِهِ

Kutoka kwa ‘Abdullah bin Burayda, kutoka kwa baba yake amesema:alikuwa Mjumbe wa Allāh ﷺ hadamki kwenda kwenye siku ya ‘Eidul-fitr mpaka ale, na alikuwa hali katika ‘Eidul-adh-ha mpaka arejee, na anakula katika kichinjwa chake[2]

(c) Kuswali viwanjani

عَنْ أَبِي سَعِيدٍ الْخُدْرِيِّ قَالَ: كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم يَخْرُجُ يَوْمَ الْفِطْرِ وَالْأَضْحَى إِلَى الْمُصَلَّى

Kutoka kwa Abuu Sa’id Al-khudury amesema: Alikuwa Mjumbe wa Allāh ﷺ anatoka siku ya ‘Eidul-fitr na ‘Eidul-adh-a anakwenda viwanjani kuswali[3]

(d) Kwenda kuswali kwa kutembea

Amesema Mjumbe wa Allāh ﷺ

إِذَا نُودِيَ بِالصَّلَاةِ فَأْتُوهَا وَأَنْتُمْ تَمْشُونَ

Itakaponadiwa swala, basi iendeeni na ilihali mnatembea[4]

(e) Wanawake kuhudhuria katika Muswala wa ‘Eid

أُمُّ عَطِيَّةَ:أُمِرْنَا أَنْ نَخْرُجَ، فَنُخْرِجَ الْحُيَّضَ، وَالْعَوَاتِقَ، وَذَوَاتِ الْخُدُورِ: فَيَشْهَدْنَ جَمَاعَةَ الْمُسْلِمِينَ وَدَعْوَتَهُمْ، فَأَمَّا الْحُيَّضُ يَعْتَزِلْنَ مُصَلَّاهُمْ

Kutoka kwa Ummu ‘Atwiyyah amesema: Tumeamrishwa kutoka na kuwatoa wenye hedhi, vigori na wenye stara zao, washuhudie umoja wa waislam na ulinganizi wao, ama wenye hedhi watajiepusha na sehemu ya kuswalia[5]

---

[1] Sunanu An-nasāi, Hadithi na. 1560
[2] Musnad Ahmad, Hadithi na. 22984
[3] Sahiihul-Bukhāry, Hadithi na. 913
[4] Sahiihu Muslim, Hadithi na. 602
[5] Sahiihul-Bukhāry, Hadithi na. 938

(f) Kubadili njia

عن جَابِرٍ قَالَ: كَانَ النَّبِيُّ صلى الله عليه وسلم، إِذَا كَانَ يَوْمُ عِيدٍ، خَالَفَ الطَّرِيقَ

Kutoka kwa Jābir amesema: Alikuwa Nabii ﷺ inapokuwa siku ya ‘Eid, anabadili njia[1]

3. **Kukithirisha matendo mema ndani yake, sababu ni miongoni mwa masiku kumi ya Dhul-hijja ni siku tukufu zaidi mbele ya Allāh ﷻ**
4. **Kupongezana katika Siku hiyo**

قال أحمدُ، رحمه الله: ولا بَأْسَ أن يقولَ الرَّجُلُ لِلرَّجُلِ يَوْمَ العِيدِ: تَقَبَّلَ اللهُ مِنَّا ومِنْكَ

Amesema Imām Ahmad – Allāh amrehemu: Na hakuna ubaya mtu kumwambia mwenzake siku ya ‘Eid: Taqabbala llāhu minnā wa minka – Allāh atukubalia sisi na wewe[2]

SIKU ZA TASHRIIQ

Masiku ya Tashriiq ni siku ya kumi na moja, kumi na mbili na kumi na tatu ya Mwezi wa Dhul-hijja. Na yameitwa Masiku ya Tashriiq sababu walikuwa wakianika nyama za wanyama waliowachinja ndani ya masiku hayo.

<u>Yanatakiwa kufanywa na kutofanywa katika Masiku ya Tashriiq</u>

(i) Masiku ya Tashriiq ni masiku maalum ambayo inasuniwa kufanya dhikri ndani yake. Anasema Allāh ﷻ:

﴿ ۞ وَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ فِيٓ أَيَّامٖ ﴾ البقرة [203]

Na mtajeni Allāh katika masiku maalum (Al-baqara, Aya 203)

Amesema Imām Al-baghawiy:

قَوْلُهُ تَعَالَى: وَاذْكُرُوا اللَّهَ، يَعْنِي: التَّكْبِيرَاتِ أَدْبَارَ الصَّلَاةِ وَعِنْدَ الْجَمَرَاتِ، يُكَبِّرُ مَعَ كُلِّ حَصَاةٍ وَغَيْرِهَا مِنَ الْأَوْقَاتِ، فِي أَيَّامٍ مَعْدُودَاتٍ الْأَيَّامُ الْمَعْدُودَاتُ هِيَ أَيَّامُ التَّشْرِيقِ وَهِيَ أَيَّامُ مِنًى وَرَمْيِ الْجِمَارِ، سُمِّيَتْ مَعْدُودَاتٍ لِقِلَّتِهِنَّ

Na kauli yake Allāh: “Mtajeni Allah” anakusudia takbiira za baada ya swala, na wakati wa kurusha mawe anatoa takbiira kalika kila jiwe na nyinginezo katika nyakati katika masiku yenye kuhesabika. Na masiku yenye kuhesabika ni masiku masiku ya Tashriiq, nayo ni masikuya mina, yameitwa yenye kuhesabika kwasababu ya uchache wake[3]

(ii) Kuchinja

(iii) Kutofunga ndani yake ila mwenye kufanya hajji ya tamat’u na hakuwa na mnyama

عَنِ ابْنِ عُمَرَ رضي الله عنهما قَالَ: لَمْ يُرَخَّصْ فِي أَيَّامِ التَّشْرِيقِ أَنْ يُصَمْنَ، إِلَّا لِمَنْ لَمْ يَجِدِ الْهَدْيَ

Kutoka kwa Ibnu ‘Umar – Allah amridhie amesema: Haikuruhusiwa katika Masiku ya Tashriiq kufunwa isipokuwa kwa asiyepata mnyama wa hajji[4]

---

[1] Sahiihul-Bukhāry, Hadithi na. 943
[2] Almughniy, Juzuu Juzuu 3 Uk.294
[3] Ma’ālim At-tanziil, Juzuu 1 Uk. 261
[4] Sahiihul-Bukhāry, Hadithi na. 1894

(iv) Kufanya matendo ya hajji yaliyobakia, kamavile: kurusha mawe jamarāt, kutufu ka’aba n.k.

FIOHI YA MAKUSUDIO YA IBADA HIZI TUKUFU

Ukitizama ibada zote hizi tukufu zinarejea katika kusudio la kuumbwa mwanaadam, ambalo ni kumpwekesha Allāh pekee na bila kumshirikisha na chochote. Na hilo tunalipata pale ambapo Allāh alipokuwa akiamrisha ibada ya Hajj na kuchinja. Akasema

﴿ وَأَتِمُّواْ ٱلۡحَجَّ وَٱلۡعُمۡرَةَ لِلَّهِۚ ﴾ البقرة [196]

Na timizeni hajj na umra kwaajili ya Allāh (Al-baqara, Aya 196)

﴿ لَن يَنَالَ ٱللَّهَ لُحُومُهَا وَلَا دِمَآؤُهَا وَلَٰكِن يَنَالُهُ ٱلتَّقۡوَىٰ مِنكُمۡۚ ﴾ الحج [37]

Na haimfikii Allāh nyama zake na wala damu yake, isipokuwa inamfikia yeye uchamungu wenu (Al-hajj, Aya 37)

Aya hizi zinadhiirisha kuwa Allāh anataka apwekeshwe katika ibada, na wala manufaa mnayoyapata nyinyi katika neema alizokuneemesheni hazimfikii bali uchamungu na ikhalsi zenu ndio zinamfikia. Hii ni tanbihi mtu akiwa anafanya ibada ajiwekee mbali na shirki, na ria ambazo hubatilisha matendo yake.

Vilevile ibada hizi zinatukumbusha siku ambayo tutarejea kwa Allāh ili kulipwa yale tuliyoyatenda. Tazama siku ya ‘Arafa namna mahujaji ambavyo wamesamama katika viwanja vya ‘Arafāt wakiwa katika vazi moja, si tajiri wala masikini. Hili linatukumbusha namna tutakavyofufuliwa tukiwa katika hali sawa na katika kiwanja kimoja

عَنِ النَّبِيِّ صلى الله عليه وسلم قَالَ: (إِنَّكُمْ مَحْشُورُونَ حُفَاةً عُرَاةً غُرْلًا)

Kutoka kwa Nabii amesema ﷺ, “Hakika nyinyi mtafufuliwa mkiwa peku, watupu, hamjatahiriwa”[1]

Hivyo ni jambo la muhimu na busara kuwa na maandalizi madhubuti ya kuzifanya ibada kwa juhudi kubwa ili kujiandaa na kukutana na mola wetu mlezi. Anasema Allāh ﷻ:

﴿ فَمَن كَانَ يَرۡجُواْ لِقَآءَ رَبِّهِۦ فَلۡيَعۡمَلۡ عَمَلٗا صَٰلِحٗا وَلَا يُشۡرِكۡ بِعِبَادَةِ رَبِّهِۦٓ أَحَدَۢا ١١٠ ﴾ الكهف [110]

Basi na yeyote anayetarajia kukutana na mola wake mlezi, basi atende matendo mema na wala asimshirikishe Mola wake mlezi na yeyote (Al-kahf, Aya 110)

[1] Sahiihul-Bukhāry, Hadithi na. 3171

Haya ni machache ambayo nimewafiqishwa kuyakusanya yenye kufungamana na masiku haya kumi na masiku ya Tashriiq. Sala na salamu zimfikie mjumbe wa Allāh na wafuasi wake wote mpaka siku ya Qiyama

---

Imekusanywa usiku wa Alhamisi, 27 Dhul-qi'idah 1447 = 14/05/2026
Zanzibar, Tanzania
+255 772 808 543/ +255 714 036 096